# TARGETER WINGS

## JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT

## GREDI YA NANE - 2024

Wings 002

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dakika 20**

**Jina** ____________________

**Shule** ____________________

**Nambari ya Usajili:** __________________ **Tarehe** __________

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.*

*(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.*

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **Upeo wa alama** | **Alama ya mwanafunzi** | **Kiwango cha utendaji** |
| 1-29 | Alama 50 | | |
| **Jumla** | **50** | | |

**I. UFAHAMU WA KUSOMA**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 4:***

Bintiye Fisi alikuwa mrembo wa ajabu. Alikuwa angali shuleni kwa masomo yake. Alitarajia kujiunga na shule ya upili mwaka uliopita. Alitaka asome hadi kiwango cha juu cha elimu ili baadaye awafae kwa hali na mali, wazazi wake waliokuwa maskini hohehahe. Hata hivyo, wazazi nao walikuwa na mawazo tofauti. Waliamua kumtilia kitumbua chake mchanga.

Bintiye Fisi anaikumbuka siku hiyo kana kwamba ilikuwa jana. Shule zilikuwa zimefungwa kwa likizo ya Disemba na ilikuwa fursa nzuri kwa wanyama wote kutangamana na watoto wao. Kama ilivyokuwa kawaida, Mzee Fisi hakukosa wageni nyumbani kwake. Baada ya kutoka mawindoni na mama yake, bintiye fisi alimkuta baba yake wakipiga gumzo na shangazi yake. Saa chache baadaye nyanya yake naye akawa mgeni nyumbani kwa Mzee Fisi kulikoni?

Jioni hiyo nyanya aliwakusanya wote mezani. 'Kama mnavyoona, mjukuu wangu amechuchuka; sasa anapaswa kutafutiwa mume'. Nyanya alieleza. 'Kwa muda mrefu sasa, ukoo wetu hujamwoza binti yeyote. Hatujala minofu kwa muda mrefu. Tumeguguna mifupa sasa naona meno yatatoka tubaki vibogoyo.'Ukoo wote uliokuwa mezani ulimshangilia nyanya. Wote wakaridhia matakwa ya nyanya. Bintiye fisi akawa sawa na kondoo anayepelekwa kichinjioni bila hiari.

Asubuhi iliyofuata fisi mmoja mkongwe aliwasili kwa Mzee fisi. Alipokelewa kwa shangwe na nderemo. Alisindikizwa na nyani aliyekuwa amekula chumvi nyingi. Bintiye fisi akaozwa kwa jikizee lililozidi baba yake kwa umri. Mfalme simba alipopata habari hizi, aliapa kuwachukulia wote waliohusika hatua kali. Alidai kuwa mila na desturi hizo zilikuwa zimepitwa na wakati.

1. Lengo la bintiye fisi masomoni ilikuwa lipi?

____________________

2. Hadithi hii inaonyesha kuwa wanyama wanaendeleza unyanyasaji wa kijinsia na ukiukaji wa haki. Je, ni mfano gani katika kifungu unaothibitisha kauli hii?

____________________

3. Je, ni jambo gani linaloonyesha kuwa mfalme Simba aliwajibikia majukumu yake?

____________________

4. Unafikiri ni kwa nini hasa nyanya alitaka mjukuu wake aozwe?

____________________



CamScanner

2. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 5 hadi 8.***

Wanafunzi walio na mahitaji maalum wanastahili kupendwa na kusaidiwa bila kubaguliwa au kupendelewa shuleni. Wanafunzi wana uwezo mkubwa wa kuwafaa wenzao bila kujali umri au jinsia. Jambo muhimu zaidi ni kuwahudumia panapohitajika. Anayetumia kitimaguru avuswhe barabarani na kusaidiwa kufika anakotaka kwenda. Hatuwezi kamwe kuvalia miwani tukamwangalia akihangaika akijisukuma kwa kitimaguru chake. Jamani! Huo sio utu.

Wanafunzi wana jukumu la kubadili mitazamo hasi ya jamii kuhusu jinsi ya kuishi na watu wenye mahitaji maalum. Wanafunzi wakusudie kuwafanya wenye mahitaji maalum kuhisi wanapendwa. Wahisi kwamba wenzao wanawajali ili ***mtagusano*** shuleni uwe ni wa ***kuridhisha***. Wanaojaribu kuwanyanyasa wachukuliwe hatua, udugu ni kufaana si kufanana.

Wanafunzi wenye mahitaji maalum ni wa aina mbalimbali: Wapo wanaotembea kwa mikongojo kwa kuzaliwa na kasoro au wengine wakapatwa na ajali. Tuwasaidie madarasani, wanapotaka kwenda haja msalani au wanapotaka kucheza. Kucheza nao kutawafanya kujihisi wao ni sehemu ya jamii ya shule. Wapo wasioweza kuona maandishi yaliyo mbali. Wasaidiwe pia. Mwalimu pia anaweza kumfaa kwa kumweka aketi kiti cha mbele ili aweze kuona vizuri. Wanafunzi wanapaswa kufahamu kuwa akufaayé kwa dhiki ndiye rafiki.

5. Ni jambo gani wanalopaswa kufanyiwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu?

_______________________________________________

6. Ni jambo lipi lisiloonyesha utu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.
   A. Kumsaidia mlemavu kupata huduma muhimu.
   B. Kuadhibu wanaonyanyaswa na walio na mahitaji maalumu.
   C. Kutompuuza mwenye mahitaji maalumu anapohangaika.
   D. Kuelimisha jamii kuishi na wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

7. Darasani mwako mna mwanafunzi aliye na tatizo la kuona; hawezi kuona mbali na anataabika kuona ubaoni. Je, utamsaidiaje mwanafunzi huyo?

_______________________________________________

8. Neno 'kuridhisha' imetumika katika kifungu hiki. Kisawe chake ni
   A. kupendezwa B. kushughulikiwa C. kutosheleza D. kuaminika.

## II. UFUPISHO

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali 9 hadi 12.***

Kila mara mtu anapomeza tembe au dawa yeyote yenye uwezo wa kusisimua sehemu za ubongo, mtu huyo huhisi msisimko.

Baadhi ya dawa tunazotumia ni zile tunazopatiwa na daktari au kuzinunua kwa agizo la tabibu. Dawa zinapaswa kutumiwa kwa njia ifaayo kwani matumizi yasiyofaa ya dawa huathiri mtumiaji wa dawa hizo. Kwa kweli, mazoea yana taabu. Matumizi ya mara kwa mara ya dawa humfanya mtumiaji kuwa mraibu wa dawa hizo. Matumizi yaliyokithiri ya dawa bila ushauri wa daktari husababisha madhara mengi na makubwa kwa mtumiaji.

Kutumia kiwango kikubwa cha dawa kuliko ilivyopendekezwa na daktari, au kutumia kiasi kidogo tu cha kiasi kilichopendekezwa ni matumizi yasiyofaa ya dawa. Zaidi ya hayo, kutumia dawa za mwenzako anayeugua ugonjwa unaofanana na wako ni hatari. Aidha kujinunulia dawa kutoka famasi bila ushauri wa daktari ni jambo lisilofaa. Hali hii imewafanya watu kuaga dunia au kupatwa na magonjwa mengine ambayo hawakuwa wakiugua hapo awali kama vile shinikizo la damu.

Matumizi yafaayo ya dawa yanapaswa kuzingatiwa na kila mmoja wetu. Tukifanya hivyo, tutaishi maisha marefu yasiyo na taabu za magonjwa. Ni kweli ulio wazi kuwa matumizi yasiyofaa ya dawa ni janga linalotukodolea macho.

9. Kifungu hiki kinahusu nini?

_______________________________________________

10. Aya ya tatu inahusu nini? Eleza kwa sentensi moja

_______________________________________________

11. Kauli, "matumizi yaliyokithiri ya dawa bila ushauri wa daktari husababisha madhara mengi na makubwa" imetumiwa katika kifungu hiki. Fupisha kauli hii kwa maneno yasiyozidi 5

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________



CamScanner

12. Andika ujumbe wa aya ya mwisho kwa sentensi moja.

______________________________________________

## III. SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 13 hadi 17. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Ni jambo la ajabu kuona jinsi teknolojia ya kisasa __13__ mambo ulimwenguni. __14__ mambo hayo ni kama vile usalama, mawasiliano, elimu na mengineyo. Hata hivyo, teknolojia hii pia ina __15__ yake kwa wanaoitumia kwa njia __16__. Kwa hivyo, kila mwanadamu anashauriwa kutumia teknolojia kwa njia __17__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13. | A. inayorahisisha | B. inarahisisha | C. inavyorahisisha | D. iliyorahisisha |
| 14. | A. Jumla ya | B. Kati ya | C. Baadhi ya | D. Katikati ya |
| 15. | A. madhara | B. ubaya | C. uharibifu | D. athari |
| 16. | A. isofaa | B. isiyofaa | C. ifaayo | D. isiofaa |
| 17. | A. inayonufaishwa | B. inayokunufaisha | C. inayowanufaiza | D. inayomnufaisha |

**Kutoka swali la 18 had 27, jibu swali kulingana na maagizo**

18. Pigia mstari kiwakilishi cha idadi katika sentensi:
Matunda sita yameiva japo kadhaa yangali mabichi

19. Sentensi: 'Wachezaji watakuwa wamekamilisha mechi yao mtakapowasili' ipo katika wakati na hali gani? ______________________________

20. Badilisha sentensi ifuatayo kutoka usemi halisi hadi usemi wa taarifa:
'Tutatii maagizo ya mahakama,' seneta alisema.

______________________________________________

21. 'Pikipiki imepata ajali lakini abiria na mwendeshaji hawakuumia' Hii ni aina gani ya sentensi?

______________________________

22. **Andika wingi wa:**
Upepo umepeperusha vumbi hadi sokoni

______________________________________________

23. **Kadi ifuatayo ina nomino mbalimbali. Andika nomino ya makundi iliyo kwenye kadi hii**

| |
|---|
| **Utandawazi** |
| **Pepopunda** |
| **Baraza** |
| **Mafuta** |
| **Nyasi** |

______________________________

24. Jaza nafasi kwa kutumia kiwakilishi cha pekee ifaavyo
______________ liliondoka kabla hatujaingia. **(Yenyewe, Chenyewe, Lenyewe)**

25. Eleza namna ritifaa ilivyotumiwa katika sentensi ifuatayo:
'takupa chai na shamba' takulimia ______________________________

26. Tunga sentensi ukitumia hali ya ukubwa wa neno jicho.

______________________________________________

27. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika kauli ya kutendwa
Mwalimu amesahihisha daftari ______________________________

## IV. FASIHI

28. a) Eleza maana ya mighani (Alama 1)

______________________________________________

b) Taja vipengele vitatu vinavyozingatiwa katika uwasilishaji wa mighani

______________________ ______________________

______________________



CamScanner

c) Visasili ni nini? (Alama 1)

_______________________________________________

d) Andika sifa tatu za visasili

_______________________ _______________________

_______________________

e) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

i) Maudhui (Alama 1)

_______________________________________________

_______________________________________________

ii) Dhamira (Alama 1)

_______________________________________________

_______________________________________________

**29.** ***<u>Sehemu hii ina dondoo kutoka kwenye tamthilia moja iliyoidhinishwa kwa wanafunzi wa gredi ya 8. Jibu swali la dondoo hili</u>***

| | | |
|---|---|---|
| **Mishi** | : | Haya, simama tuone. |
| **Mabula** | : | *(Anasimama)* Wapi? Ulevi uko wapi? Mlevi asingeweza hata kusimama. |
| **Mishi** | : | Mabula, unayaamini hayo usemayo? |
| **Mabula** | : | Si umeona mwenyewe? |
| **Mishi** | : | Acha nione sasa. Hebu simama wima kwa mguu mmoja. |
| **Mabula** | : | Basi ona mwenyewe. *(Anajitahidi kusimama lakini mwishowe anashindwa na kuanguka. Mishi anamkimbilia na kwenda kumwinua).* |
| **Mishi** | : | Ona sasa! Umeumia? |
| **Mabula** | : | *(Ameinuliwa)* kwani nimeanguka kutoka ghorofani? |
| **Mishi** | : | Hujui kuwa hakuna mwiba usiokuwa na uchungu? |
| **Mabula** | : | *(Anajifanya kutazama kuta za nyumba)* Hii nyumba hii? |
| **Mishi** | : | Nyumba nayo imekufanya nini? |
| **Mabula** | : | Hizi nyumba za kubabaisha humfanya mtu kukunguwaa kwa kukosa level. Nyumba yenyewe wasiwasi kama walioitengeneza... |
| **Mishi** | : | Bila kibanda hiki leo ungeficha uso wako wapi? Ungejisitiri wapi? (Kimya kifupi) Umesahau mara? Mbona umekuwa mwepesi wa kusahau? |

a) Taja mandhari ya dondoo hili (Alama 1)

_______________________

b) Wataje wahusika wawili katika dondoo hili (alama 2)

_______________________ _______________________

c) Eleza sifa mbili za Mabula (Alama 2)

_______________________________________________

_______________________________________________

d) Fafanua masuala mawili ambayo yameshughulikiwa katika dondoo hili. (alama 2)

_______________________________________________

_______________________________________________

e) Katika dondoo hili mwandishi ametumia mbinu tofauti tofauti za lugha kuwasilisha mawazo yake. Eleza kati ya mbinu hizo (Alama 3)

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________



CamScanner

***Rafiki yako amekusaidia kutatua shida iliyokuwa ikikusumbua katika somo la Hisabati. Mwandikie barua ya kutoa shukrani kwa usaidizi wake.***



CamScanner